GPE KIX BRIEF

Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu — Ubadilishanaji wa Maarifa na Uvumbuzi

MAARIFA YA SERA

KUHUSU CHAGUO ZA ELIMU KWA WATOTO WALIO NJE YA SHULE NA WALE WENYE HATARI YA KUACHA SHULE

GPE KIX
KNOWLEDGE INNOVATION EXCHANGE

IDRC · CRDI
International Development Research Centre
Centre de recherches pour le développement international

Canada





Muunganisho wa miradi minne ya GPE KIX katika Afrika na Asia unawapatia wasimamizi wa maamuzi mikakati madhubuti na mapendekezo ya kuzuia kuacha shule na kuwaunga mkono wanafunzi walio nje ya shule.

Picha: GPE/ Translieu

Kote duniani, UNESCO inakadiria kuwa takriban watoto na vijana milioni 251 wenye umri wa kati ya miaka sita na 18 wako nje ya shule, huku mamilioni wengine wakiwa katika hatari ya kuacha shule. Ili kushughulikia mahitaji ya wanafunzi hawa walio katika mazingira hatarishi, serikali na wadau wengine wa elimu wanatafuta chaguo zinazotegemea ushahidi na zenye ufanisi wa gharama za kuongeza udumishaji shuleni na kurahisisha mpito wa kurudi katika elimu rasmi kwa wale walio nje ya shule.

Kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu — GPE (Global Partnership for Education) kupitia Ubadilishanaji wa Maarifa na Uvumbuzi — KIX (Knowledge and Innovation Exchange), iliunga mkono miradi minne ya utafiti kupima, kutathmini na kuendeleza mikakati ya kueneza uvumbuzi wa elimu unaoweza kuongeza upatikanaji wa elimu bora kwa watoto na vijana walio nje ya shule — OOSCY (Out-Of-School Children and Youth) na wale walio katika hatari ya kuacha shule.

UTAFITI

Utafiti huu, ambao ulihusisha nchi 15 barani Afrika na Asia, ulilenga:

- **Programu za Elimu ya Kasi — AEPs** (Accelerated Education Programs), ambazo huziba mapengo muhimu katika mitindo ya elimu ya jadi kwa kuwapatia OOSCY mitaala iliyobanwa, mbinu za ufundishaji zilizolengwa na ratiba nyumbufu za ujifunzaji.
- **Mbinu zilizoboreshwa za shuleni** — kama vile mafunzo bora ya walimu, ushiriki wa jamii na shughuli za ziada nje ya mtaala — kuzuia kuacha shule rasmi na kuwavutia watoto na vijana walio nje ya shule kurudi katika mfumo wa elimu.

Kila mradi ulitathmini programu mbalimbali na mbinu za shuleni, ukizidisha uelewa wa sifa zao na ubora wa utekelezaji wao. Kwa jumla, AEPs na mbinu zaidi ya 30 zilipitiwa, ambapo wanafunzi, wazazi, walimu, maafisa wa elimu na wadau wengine wakuu walitoa maoni kuhusu kinachofanya kazi na kinachohitaji kuboreshwa. Matokeo haya yalitumika kuipa serikali na wadau wengine taarifa kuhusu sera, mikakati na mbinu madhubuti ili ziweze kuigwa na kuenezwa.

Muunganisho wa matokeo kutoka miradi hii minne unaangazia sifa muhimu za AEPs zenye ufanisi, mikakati ipi inafanya kazi vizuri zaidi kuwabakiza watoto na vijana shuleni, na athari gani programu na mbinu hizi zimepata. Pia unatoa orodha ya mapendekezo kwa watunga sera, wafadhili na wengine wanaohusika katika kufanya maamuzi ya elimu.



Picha: GPE/ Salman Saeed

MIRADI MINNE YA GPE KIX ILIJUMUISHA:

Utafiti Linganishi wa Programu za Elimu ya Kasi na Mitindo ya Elimu Inayowalenga Wasichana — Comparative Study of AEPs and GFMs): Ghana, Nigeria na Sierra Leone.

Mradi wa Back2School: Kueneza Mtindo wa Ujifunzaji wa Kasi kwa Wasichana Walio Nje ya Shule katika Jamii za Vijijini — Back2School: Ethiopia, Kenya na Tanzania.

Mtindo Mpya wa Madarasa ya Kuziba Pengo kwa Kuboresha Ujifunzaji wa Watoto na Vijana Walio Nje ya Shule — Bridging Classes for OOSCY: Burkina Faso, Guinea, Côte d'Ivoire, Mali, Niger na Senegal.

Ufanisi na Uwezo wa Kueneza wa Programu kwa Watoto Walio Nje ya Shule na Walio katika Hatari ya Kuacha Shule — Scalability of Programs for OOSCY and At-Risk Learners: Bangladesh, Bhutan na Nepal.

SIFA MUHIMU ZA AEPS ZENYE UFANISI

Katika mazingira tofauti, sifa zifuatazo muhimu za programu zilithibitika kuwa na ufanisi katika kukidhi mahitaji mbalimbali ya OOSCY:

- **Kasi:** Kufunika mtaala kwa haraka zaidi ni jambo lenye ufanisi wa gharama kwa serikali na linavutia kwa wazazi na wanafunzi wakubwa walioshindwa kupata stadi za msingi za ujifunzaji.
- **Unyumbufu:** Ratiba nyumbufu za ujifunzaji, zilizorekebishwa kulingana na shughuli za jamii na za kiuchumi, huwawezesha watoto na vijana wengi zaidi kuhudhuria shule.
- **Ushiriki wa wazazi na jamii:** Kujenga uelewa miongoni mwa wazazi na jamii kuhusu thamani ya elimu kunaweza kubadilisha kanuni za kijamii na kitamaduni zinazowafanya watoto na vijana wabaki nje ya shule.
- **Gharama nafuu:** Kufidia ada za shule na kutoa nyenzo za ujifunzaji — na katika baadhi ya matukio chakula, usafiri na taulo za hedhi — ni motisha kubwa kwa ushiriki katika ujifunzaji wa kasi.
- **Mbinu za kufundisha zinazomzingatia mwanafunzi:** Mbinu za ufundishaji zinazomzingatia mwanafunzi huongeza umakini wa wanafunzi na hufanya ujifunzaji wao uwe na umuhimu zaidi.
- **Ufundishaji unaotegemea lugha ya mama:** Kujifunza kwa lugha ya mama hurahisisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, na huongeza maarifa na kujiamini kwa wanafunzi.
- **Walimu na wawezeshaji katika jamii:** Kuwa na wawezeshaji na walimu katika jamii kunaweza kuboresha wanafunzi kuendelea kupata masomo katika maeneo ya mbali au yaliyoathiriwa na migogoro na kuongeza uelewa wa vikwazo vya kielimu vya eneo husika.

MIKAKATI YA KUZUIA KUACHA SHULE

Mikakati ifuatayo ilibainika kuwa na ufanisi katika kupunguza viwango vya kuacha shule:

- Kampeni za kujenga uelewa na kushirikisha jamii na wazazi ili kuwaunganisha vyema na walimu na shule, na kuongeza uwezo wa wazazi wa kushiriki na mfumo wa elimu.
- Shughuli zilizoboreshwa za ziada nje ya mtaala shuleni ili kuboresha udumishaji wa wanafunzi, kupunguza kuacha shule na kuongeza shauku ya wanafunzi, ushiriki na hisia ya kuwa wamekubalika shuleni.
- Warsha na matukio ya usawa na ujumuishaji shuleni kuhusu mada kama vile usafi wa hedhi, afya na usafi wa msingi, unyanyasaji wa kingono na kupinga uonevu ili kustawisha usawa wa kijinsia, ujumuishaji wa kijamii na mazingira salama zaidi ya shule.
- Kuimarisha uwezo wa walimu katika mikakati ya kufundisha na kujifunza inayotegemea uzoefu na ya teknolojia ya habari na mawasiliano — ICT (Information and Communication Technology).
- Juhudi binafsi za wanafunzi wenye ulemavu, kupitia ushirikiano kati ya shule na mashirika ya kienyeji

ATHARI YA AEPS NA MBINU ZA SHULENI KWA JAMII ZILIZO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI

Miradi hii minne ilionyesha jinsi AEPs na mbinu zilizoboreshwa za shuleni zinavyoweza kuboresha upatikanaji wa elimu, udumishaji shuleni na matokeo ya ujifunzaji kwa vijana walio katika mazingira hatarishi — mara nyingi kwa fedha kidogo zaidi kuliko utoaji wa shule rasmi. Kwa kutegemea mapitio yao ya AEPs zilizopo au za zamani na majaribio yao ya marekebisho au uvumbuzi wa AEP, matokeo yafuatayo yalibainika:

1. **Kuongezeka kwa upatikanaji wa elimu kwa jamii zilizotengwa:** Nchini Nigeria, takriban OOSCY 310,000 walipata elimu kwa miaka saba kupitia AEPs tano zilizopo, na hivyo kuwapatia wanafunzi upatikanaji wa elimu ambao kwa namna nyingine usingepatikana. Nchini Nepal, kampeni za elimu kwa wazazi zilizofanyiwa majaribio kupitia utafiti zilipelekea kupungua kwa asilimia 20 kwa OOSCY na kuongezeka kwa asilimia 2 kwa usajili shuleni katika wilaya ambazo kampeni zilifanywa.

2. **Viwango vya juu vya mpito wa kwenda elimu rasmi:** Nchini Ghana, mapitio ya programu za sasa na za zamani za elimu ya msingi ya ziada yalibaini kuwa asilimia 80 au zaidi ya wanafunzi wa AEP walifanya mpito kwenda elimu rasmi, ambapo wasichana walikuwa na viwango vya juu zaidi kuliko wavulana kutokana na uchaguzi wa makusudi wa wasichana katika programu.

3. **Maendeleo ya stadi zinazoongeza uwezeshaji wa kiuchumi:** Mapitio ya mitindo ya AEP nchini Nigeria yalibaini kuwa wanafunzi walipata stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, mawasiliano na maisha ya kila siku ambazo zilichukuliwa kuwa za thamani isiyokadirika katika maisha yao ya kazi na kuwasaidia familia zao kukidhi mahitaji ya nyumbani, kama vile kusoma ripoti za kimatibabu.

4. **Uwezeshaji wa wanafunzi, hasa wasichana:** Katika mitindo ya AEP iliyopitiwa nchini Sierra Leone, wanafunzi waliripoti uwezeshaji ulioimarishwa, kujithamini na kujiamini, kwa sehemu kutokana na mbinu za kipekee za kufundisha. Nchini Ethiopia, wazazi, walimu na jamii walibaini kuongezeka kwa kujiamini, kujithamini, nidhamu na uwajibikaji wa wanafunzi wa AEP.

5. **Utendaji wa kitaaluma unaolingana au bora kuliko shule rasmi:** Katika uvumbuzi uliofanyiwa majaribio nchini Côte d'Ivoire, Guinea na Mali, asilimia 70 ya wanafunzi wa AEP walionyesha umahiri katika lugha na mawasiliano. Katika mitindo ya AEP iliyopo iliyopitiwa nchini Sierra Leone, wanafunzi walikuwa wakilingana na wanafunzi wa shule rasmi katika kusoma maneno, huku wakipata alama za chini kidogo katika kuelewa wanachosoma.

6. **Stadi mpya na uwezo kwa walimu na wawezeshaji:** Katika utafiti kuhusu mitindo ya AEP iliyorekebishwa nchini Kenya, walimu walionyesha stadi mpya katika kusimamia wanafunzi wa elimu ya kasi ndani ya madarasa na katika kukidhi mahitaji yao mahususi, jambo lililopelekea utendaji bora wa kitaaluma.

7 **Viwango vya chini vya kuacha shule:** Nchini Bangladesh, kulikuwa na kupungua kwa asilimia 11 kwa viwango vya kuacha shule kutokana na hatua za pande nyingi zilizofanyiwa majaribio na walimu, wanafunzi na jamii.

8 **Uungwaji mkono ulio imara zaidi wa jamii na wazazi kwa elimu:** Nchini Nepal, kampeni za kushirikisha wazazi zilizofanyiwa majaribio kupitia utafiti ziliongeza maarifa, imani na uwezo wa wazazi katika kuleta mabadiliko chanya katika mazingira ya shule ya watoto wao.

9 **Viwango vya chini vya ndoa za utotoni na mimba za utotoni:** Nchini Ghana, mapitio ya mitindo ya elimu ya msingi ya ziada katika maeneo 32 ya utafiti yalibaini ushahidi wa kupungua kwa ndoa miongoni mwa wasichana wenye umri wa miaka 10-15. Wasichana katika AEPs pia walijifunza jinsi ya kuzuia unyanyasaji, shambulio na mimba.

10 **Ufanisi wa gharama:** Gharama ya kila kitengo ya programu ya Ghana ya elimu ya msingi ya ziada ya kasi katika 2019-2020 ilikuwa chini kwa asilimia 21.4 kuliko gharama ya kila kitengo ya mfumo wa kawaida, bila kujumuisha gharama ya mafunzo ya walimu. Aidha, mwaka mmoja wa elimu ya kasi unalingana na miaka 2.4 ya elimu rasmi, ikimaanisha kuwa elimu ya msingi ya ziada ina ufanisi mara mbili kuliko mfumo rasmi.



Picha: GPE/ Infinitee!

MAPENDEKEZO YA SERA

Muunganisho wa matokeo kutoka miradi hii minne ulizalisha orodha ya mapendekezo kwa wale wanaohusika katika kufanya maamuzi ya elimu na kubuni programu.

1. Ingiza programu na mbinu za elimu ya kasi na mbadala katika bajeti za serikali ili kuwezesha uenezaji na kuhakikisha uendelevu.
2. Endeleza sera, miongozo, viwango vya ubora na mitaala iliyolinganishwa na inayozingatia jinsia kwa AEPs, kwa kutegemea sifa na mbinu muhimu zilizothibitika kuwa na ufanisi.
3. Tumia shule kuunga mkono uelewa na utekelezaji wa sheria za kulinda watoto, kama vile zile zinazohusu usafirishaji haramu wa watoto na ndoa za utotoni.
4. Imarisha uhusiano kati ya AEPs na shule rasmi na panua njia za ujifunzaji kwa wanafunzi wa elimu ya kasi zaidi ya elimu ya msingi ili kujumuisha mafunzo ya ufundi na stadi.
5. Imarisha programu katika shule rasmi zinazounga mkono upatikanaji na udumishaji kwa wanafunzi walio katika mazingira hatarishi na kuzuia kuacha shule.
6. Boresha miundombinu ya shule na unga mkono elimu inayopatikana na jumuishi kwa watu wenye ulemavu.
7. Wekeza katika uajiri, mafunzo na maendeleo ya kitaaluma ya walimu na wawezeshaji, kwa kuzingatia hasa wanawake.
8. Kusanya takwimu kamili kuhusu OOSCY na AEPs — ikiwa ni pamoja na jinsi jinsia inavyoingiliana na vipengele vingine vya idadi ya watu na vya kimazingira — ili kuunga mkono ufanyaji wa maamuzi unaoendelea unaotegemea ushahidi.
9. Ifanye jamii kua kitovu cha maboresho ya chaguo za elimu kwa OOSCY na wale walio katika hatari ya kuacha shule.

Maarifa haya ya sera yametolewa kutoka katika ripoti ya 'Education Options for Out-of-School Children and Those at Risk of Dropping Out: A Research Synthesis' (Chaguo za Elimu kwa Watoto Walio Nje ya Shule na Wale Wenye Hatari ya Kuacha Shule: Muunganisho wa Utafiti).

GPE KIX ni juhudi ya pamoja kati ya GPE na IDRC (International Development Research Centre — Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Maendeleo) yenye lengo la kuhakikisha nchi washirika zinapata na kutumia ushahidi na uvumbuzi wanaohitaji ili kuharakisha upatikanaji, matokeo ya ujifunzaji na usawa wa kijinsia kupitia mifumo ya elimu yenye usawa, jumuishi na yenye uwezo wa kustahimili changamoto, inayofaa kwa karne ya 21.

Ripoti tano za muunganisho ziliagizwa na GPE KIX kuunganisha ushahidi katika miradi ya utafiti iliyofanyika kati ya 2020 na 2024 kuhusu mifumo ya takwimu na matumizi ya takwimu; ujifunzaji wa awali; usawa wa kijinsia, usawa na ujumuishaji; maendeleo ya kitaaluma ya walimu; na watoto na vijana walio nje ya shule.

GPE KIX KNOWLEDGE INNOVATION EXCHANGE

IDRC · CRDI

Canada